**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**
**STASHAHADA YA UALIMU WA SEKONDARI**

**721** **KISWAHILI**

**Time: 3 Hours** **MAJIBU** **Year: 2024**

---

**Instructions.**

1. This paper consists of sections A and B with a total of **Fourteen (14)** questions.
2. Answer **all** questions from section A and **four (4)** questions from section B.
3. Section A carries **forty (40)** marks and section B Carries **sixty (60)** marks.
4. Cellular phones are **note** allowed in the examination room.
5. Write your **examination Number** on every page of your answer booklet(s).

maktaba.tetea.org
TETEA

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali yote katika sehemu hii. Kila swali lina alama **Nne (4).**

1. (a) Tofautisha Nomino za pekee na Nomino dhahania.
**Nomino za pekee** ni aina ya maneno yanayotaja majina yenye sifa za pekee kama vile mahali, majina ya watu mfano Asha wakati **Nomino za dhahania** ni aina ya nomino inayotaja majina ya vitu vya kudhaniwa visivyoonekana kama vile Mungu na njaa.

(b) Tofautisha Vivumishi vya a–unganifu na Vivumishi vya jina kwa jina.
Vivumishi vya a-unganifu ni aina ya vivumishi vinavyoelezea sifa ya nomino bayana vilivyoundwa na maneno ya aunganifu mfano maziwa ya mtoto wakati vivumishi vya jina kwa jina ni aina ya vivumishi vinavyotaja sifa ya nomino kwa mtindo wa jina mfano Bata mzinga.

2. Bainisha vipengele vinne vya andalio la somo vilivyopo nje ya hatua za somo vinavyodokeza taarifa mbalimbali zinazomgusa mwanafunzi.

- idadi kamili ya wanafunzi,
- tathmini ya wanafunzi,
- kipengele cha malengo mahsusi
- kipengele cha maoni.

3. Chunguza sentensi kwa makini, kisha kubainisha kila sentensi kuwa ni aina gani ya tamathali za semi:
(a) Juma ni simba - **sitiari**
(b) Juma ni shupavu mithili ya simba dume - **tashibiha**
(c) Miti ilirukaruka kwa furaha - **tashihisi**
(d) Dada yangu amejifungua mtoto wa kiume. - **tasfida**

4. Kwa kutumia hoja nne, dhihirisha uhusiano uliopo kati ya zana na vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

- zana na vifaa vyote hutumiwa na mwalimu na mwanafunzi katika kujifunza,
- zote zinatumika kulingana na somo, umri, idadi na uwezo wa mwanafunzi,
- ili zana itengenezwe lazima pawepo na vifaa,
- zote zinaratibiwa na mtaala katika suala zima la ufundishaji na ujifunzaji.

5. kuchunguza kwa makini maneno popo, chungwa, nanasi, kiwanda, beba, dhahabu, ng`ambo, na fuvu kisha kujibu maswali yafuatayo:
(a) kuorodhesha maneno yenye konsonanti zinazotamkwa kwa kukutanisha mdomo wa chini na wa juu
(b) kueleza kwa ufupi sifa za konsonanti zinazounda maneno hayo kwa kuzingatia namna ya matamshi.

(a) Popo na beba
(b) Konsonanti p na b huitwa vipasuo ambapo katika utamkaji wake ala za sauti hukutana na huzuia mkondo wa hewa na baadae kuachiwa ghafla

6. Fafanua ngazi nne za jazi la uelekeo atakazotumia Mwalimu Chipa kuandaa mtihani wa Kanda kwa wanafunzi wa Kidato cha Pili.

- Ngazi ya kuwa tayari kupokea – inahusu namna mwanafunzi anavyokuwa tayari

- kujifunza au kupokea maarifa, ngazi ya kuitikia – hupima jinsi mwanafunzi anavyoweza kushirikiana

- katika kujifunza, ngazi ya kuthamini – hupima uwezo wa mwanafunzi kujithamini mwenyewe na

- kuthaminisha watu na vitu, ngazi ya kuwianisha – hupima uwezo wa mwanafunzi kulinganisha na kutofautisha vitu.

7. Taja mambo manne ya kuzingatia katika ufahamu wa kusikiliza.

    - kuwa makini na Habari inayosomwa,
    - kubaini wazo kuu katika habari hiyo,
    - kutambua kichwa cha habari,
    - kubaini misemo, vifupisho na matumizi ya lugha yaliyotumika katika habari hiyo.

8. Thibitisha kwa kutumia hoja nne juu ya manufaa ya insha zinazotetea mawazo ya aina fulani na kupinga mawazo mengine.

    - insha huongeza maarifa kwa wasomaji juu ya mambo mbalimbali,

    - insha hizi huongeza uwezo wa kuchambua hoja kwa wasomaji yaani hoja za msingi na zisizo za msingi,

    - insha huongeza uwezo wa kufikiri kwa wasomaji jinsi ya kutetea na kupinga hoja,

    - insha hukuza na kuendeleza stadi za kusoma kwa wasomaji.

    - insha za hoja hukuza uelewa kwa msomaji kwa kuwa msomaji hutambua lipi jema na lipi baya,

    - insha humjengea msomaji ujasiri wa kujieleza kwani anaposoma

    - insha anapata uwezo wa kujieleza kimantiki, humpa msomaji motisha ya kuendelea kusoma kazi hizo, humsaidia msomaji kujitambua vema na kufanya maamuzi sahihi katika maisha.

9. Eleza manufaa manne ya mwalimu kufanya upimaji wa wanafunzi wakati wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

    - kujua maendeleo ambayo yamefikiwa na mwanafunzi wakati wa ujifunzaji wa mada husika, kumsaidia mwalimu kuboresha zana za ufundishaji na ujifunzaji,

    - kumsaidia mwalimu kubaini changamoto mbalimbali ambazo huwapata wanafunzi wakati wa ujifunzji,

    - kumsaidia mwalimu kuboresha mbinu za kufundishia na kujifunzia.

- upimaji huwasaidia wanafunzi kuvuka ngazi moja ya elimu kwenda ngazi nyingine mfano mtihani wa darasa la saba,

- upimaji hukuza na kuchochea ari ya kusoma na huleta ushindani mzuri mfano mitihani ya muhula,

- upimaji unasaidia kutoa taarifa ya maendeleo ya mwanafunzi kwa mzazi au mlezi mfano mitihani ya kufunga mwaka,

- upimaji husaidia wanafunzi kupata ajira maeneo mbalimbali mfano benki.

10. Tunga sentensi moja kwa kila kiwakilishi cha nafsi kama ifuatavyo;

(a) Kiwakilishi cha nafsi ya kwanza wingi
(b) Kiwakilishi cha nafsi ya tatu umoja
(c) Kiwakilishi cha nafsi ya pili wingi
(d) Kiwakilishi cha nafsi ya kwanza umoja.

(a) Sisi tunaimba wimbo wa Shule
(b) Yeye anacheza mpira wa miguu
(c) Ninyi mnapika vizuri sana
(d) Mimi ninapenda kula ugali na samaki.

**SEHEMU B (Alama 60)**

Jibu maswali **yote** kutoka sehemu hii. Kila swali lina alama **kumi na tano (15).**

11. Tumia ithibati tano za kihistoria kukubaliana na kauli kwamba, "Kiswahili ni Kibantu kwa asili yake".

ushahidi wa kihistoria wa mji wa Kilwa;
Wageni walipofika eneo hilo walikuta wenyeji wakimwita Sultani wa Kilwa kwa majina ya utani kama vile " mkoma watu" na " nguo nyingi";

Wageni walipokuja Afrika Mashariki walikuta watu wakiimba nyimbo ambazo zilitumia lugha za Kibantu kama Kimvita ambayo ni lugha ya kibantu; Mwanahistoria Ibn Batuta katika karne ya 14 BK alisema alikuja Pwani ya Afrika Mashariki na aliwakuta watu wakiishi wakiwa na utamaduni wao wa kula aina fulani ya chakula kama nafaka;

Ali-Idris naye ni mgeni aliyefika Afrika ya Mashariki na kuingia mji wa Zanzibar; Katika ujio wake


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

aligundua jina la kwanza la Zanzibar kuwa ni “Unguja”; Pia alikuta majina kama ya vifaa kama vile “Kikombe” na majina ya ndizi ambayo yanatumika hadi sasa. Kwa mfano, “mkono wa tembo”,

“Muhani wa sukari”; Al-Masudi katika maandiko yake anazungumzia kuhusu wakazi wa mwambao ambao walijulikana kwa jina la “wazanji” kwa maana hiyo inaonesha kuwa neno Zanzibar lilitokana na neno Zanjibar yaani Pwani ya

“Zanji”. Anaeleza kuwa Wazenji walikuwa na watawala wao waliotokana na “Wakilinia” ambao waliamini waliletwa na Mungu. Kuna maelezo yanayodai kuwa neno “wakilini” lina maana ya wafalme.

12. Eleza mambo matano ambayo mhakiki anapaswa kuzingatia anapohakiki kipengele cha lugha katika kazi ya fasihi.

mhakiki lazima ajue lugha mbalimbali zilizotumika katika kazi ya fasihi ili aweze kuitendea haki,

mhakiki lazima ajue semi mbali mbali kama vile nahau, methali, misemo inayotumika katika kzi za fasihi,

mhakiki lazima ajue taswira zilizotumika katika kazi ya fasihi,

mhakiki lazima azingatie lugha fasaha inayotumika katika kazi ya fasihi,

mhakiki lazima atambue tamathali za semi zilizotumika katika kazi ya fasihi mfano, tashihisi, sitiari, tafsida n.k.

13. Fafanua hatua sita za ufundishaji ambazo huzingatiwa kwa wanafunzi wanaoanza kujifunza lugha ya Kiswahili.

Ufundishaji wa stadi ya kusikiliza:
Katika stadi hii mwanafunzi anapokea sauti kutoka kwa mzungumzaji na kupata uelewa,

Ufundishaji wa stadi ya kuzungumza:
Stadi ya kuzungumza ni uwezo wa mwanafunzi kuunda matini na kuyatoa kwa mdomo,

Ufundishaji wa stadi ya kusoma:
Stadi ya kusoma ni uwezo wa mwanafunzi kutambua maumbo ya maandiko na kupata uelewa,

Ufundishaji wa stadi ya kuandika:
Stadi ya kuandika ni uwezo wa mwanafunzi kuumba matini kwa njia ya maandishi,

Ufundishaji wa kujieleza kwa kina na ufasaha:
Stadi hii ni ngazi ya juu ya uzungumzaji kwani mwanafunzi hufundishwa masuala kama vile kujenga hoja, kufafanua, kuhoji n.k,

Ufundishaji wa ufahamu: Hapa mwanafunzi hufundishwa kubaini maana za matini na kuweza kujibu maswali kutokana na matini husika ambayo amesikiliza au kusoma.

14. Bainisha vigezo sita vya kuzingatia wakati wa kutengeneza zana za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili.

- Kuendana na mada husika:
  Zana hutakiwa kuendana na mada inayolengwa kufundishwa;

- Kuendana na lengo mahususi la somo husika:
  Zana za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili hutakiwa kuendana na lengo mahususi;

- Kuendana na mazingira:
  Zana za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili hutakiwa kuakisi mazingira halisi ambamo mada inafundishiwa;

- Kuwa toshelevu:
  Zana za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili hutakiwa kuendana na idadi ya wanafunzi wanaolengwa kuitumia;

- Kutokubagua wanafunzi:
  Zana inatakiwa izingatie mipaka ya utamaduni wa jamii ambamo wanafunzi wanatokea; Kuendana na mila na desturi za jamii husika: inashauriwa mwalimu kutumia vifaa/michoro isiyokinzana na mila, desturi na tamaduni za jamii husika inayomzunguka; Zana ya ufundishaji na ujifunzaji inatakiwa

- kumfikirisha mwanafunzi:
  mwanafunzi akifikirishwa kwa zana iliyoandaliwa itamsaidia kushiriki kipindi kwa zaidi ya mlango mmoja;

- Zana inatakiwa kuvutia ili wanafunzi waweze kuwa makini na wasikivu katika kujifunza kupitia zana hiyo.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org